



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L .P 796, Simu: 255- 022 2122722/3/4
Dar es Salaam –TANZANIA

Nukushi: 255- 022 2130852
Baruapepe: dg@nbs.go.tz



TAARIFA KWA UMMA

PATO LA TAIFA KWA ROBO YA TATU YA MWAKA, 2013

Utangulizi

Pato la Taifa ni thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa nchini kutokana na shughuli za kiuchumi katika kipindi husika. Takwimu za Pato la Taifa hupima thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa nchini kutokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi katika kipindi husika. Takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka hutayarishwa kwa kipindi cha Januari – Desemba. Aidha, Takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka hutayarishwa kwa kipindi cha miezi mitatu yaani Januari – Machi, Aprili – Juni, Julai – Septemba na Oktoba – Desemba. Taarifa hii ni kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2013.

Mfumo na Uainishaji Unaotumika

Utararishaji wa Takwimu za Pato la Taifa unafuata Mfumo wa Umoja wa Mataifa (United Nations_System of National Accounts) ambao unatoa dhana kwa kina, maana na uainishaji wa shughuli za kiuchumi kwa ajili ya Takwimu za Pato la Taifa. Aidha, katika kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa, mfumo wa kimataifa wa kuainisha shughuli za kiuchumi “International Standard Industrial Classification of all Economic Activities - Rev.3” umetumika.

Mbinu zinazotumika

Utararishaji wa Takwimu za Pato la Taifa nchini Tanzania kwa kiasi kikubwa unatumia njia ya **uzalishaji bidhaa na huduma** na njia ya **matumizi**. Taarifa zinazotumika ni za uzalishaji wa bidhaa na utoaji huduma katika shughuli zote za kiuchumi nchini.

Utararishaji wa Takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka unatumia mbinu sawa na zile za Takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka. Tofauti iliyopo inatokana na wigo wa taarifa zilizotumika. Takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka hutumia taarifa zenye wigo mpana zaidi ya Takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka.


Takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka husaidia katika kufanya marekebisho muafaka ya sera mbalimbali kwa kutoa takwimu zinazoaminika na kwa wakati za mwenendo wa uchumi katika vipindi vifupi vya robo mwaka. Takwimu hizi za Pato la Taifa kwa robo mwaka hufanyiwa marekebisho inapobidi kwa kutumia taarifa mpya kutoka vyanzo mbalimbali.

Ukuaji wa Uchumi

Katika kipindi cha Julai - Septemba 2013, Pato la Taifa kwa bei za soko liliongezeka kwa kasi ya asilimia 6.5 ikilinganishwa na asilimia 7.2 kipindi kama hicho mwaka 2012 (**Chati Na. 1**).

Jumla ya thamani ya Pato la Taifa katika kipindi husika mwaka 2013 ilikuwa Sh. trilioni 5.9 ikilinganishwa na Sh. trilioni 5.5 mwaka 2012.

Chati Na. 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa Robo ya Tatu, Mwaka 2003-2013



Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi

(i) Kilimo

Shughuli za kiuchumi za Kilimo cha mazao, mifugo, misitu na uwindaji ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 6.1 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 5.7 ya kipindi kama hicho mwaka 2012. Katika kipindi hiki, mahindi yaliyozalishwa yaliongezeka kwa asilimia 7.1 kutoka tani milioni 5.1 zilizozalishwa katika robo ya tatu ya mwaka 2012 hadi tani milioni 5.5 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Mpunga uliozalishwa uliongezeka kwa asilimia 7.5 kutoka tani milioni 1.5 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2012 hadi tani milioni 1.6 zilizozalishwa katika kipindi husika mwaka 2013. Kiasi cha Mtama na Uwele kiliongezeka kwa asilimia 13.0 kutoka tani milioni 1.0 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2012 hadi tani milioni 1.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Mihogo iliyozalishwa iliongezeka kwa asilimia 9.4 kutoka tani milioni 3.9 zilizozalishwa katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2012 hadi tani milioni 4.3 katika kipindi husika mwaka 2013. Ukuaji huu ulitokana na kuwepo kwa mvua za kutosha katika maeneo yanayozalisha mazao ya kilimo kwa wingi na juhudi za Serikali za kukuza uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo.

(ii) Uvuvi

Shughuli za Uvuvi zinahusika na uvunaji wa samaki kutoka katika maziwa, mabwawa, mito na bahari. Shughuli za uvuvi ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 3.1 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 1.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2012.

Kasi ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya samaki na mazao yake katika soko la ndani na soko la kimataifa.

(iii) Uchimbaji Madini na Mawe

Shughuli hii ya kiuchumi inahusu ukusanyaji au uchimbaji wa madini, vito vya thamani na mawe kutoka juu au chini ya ardhi. Shughuli hii iliongezeka kwa kasi ya asilimia 10.4 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 1.3 kipindi kama hicho mwaka 2012. Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka 2013 Kilo 10,189 za Dhahabu zilizalishwa ikilinganishwa na Kilo 9,509 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Tanzanite iliyozalishwa katika robo ya tatu ya mwaka 2013 iliongezeka na kufikia Kilo 5,140 kutoka Kilo 3,913 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Kasi ya kuongezeka ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya Dhahabu na Tanzanite.

(iv) Uzalishaji Viwandani

Shughuli za Uzalishaji Viwandani zinahusika na kuchakata mali ghafi kwa lengo la kupata bidhaa za mwisho kwa ajili ya matumizi au kupata bidhaa za kati kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa nyingine. Shughuli hii ilikua kwa kasi ya asilimia 5.8 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 11.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Aidha, kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa nyingine za vyakula, bidhaa za kemikali na uzalishaji wa sementi.

(v) Umeme, Gesi na Maji

Shughuli hii ya kiuchumi inahusika na uzalishaji wa umeme kutoka vyanzo mbalimbali kama vile maji, gesi asilia, nishati ya jua na mafuta pamoja na usambazaji wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Shughuli hii ilikua kwa kasi ya asilimia 2.3 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 7.6 katika kipindi husika mwaka 2012. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa shughuli ya uzalishaji wa umeme, gesi na maji kulitokana na kupungua kwa umeme uliozalishwa kufuatia kufungwa kwa muda visima vya gesi asilia huko Songo Songo kwa ajili ya kuvisafisha.

(vi) Ujenzi

Shughuli za kiuchumi za ujenzi zinahusika na kusafisha maeneo kwa ajili ya ujenzi, ujenzi wa nyumba, barabara, madaraja na miundombinu ya kusambaza gesi, nishati ya umeme na maji. Shughuli za ujenzi ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 7.3 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 6.5 kipindi kama hicho mwaka 2012. Ongezeko hili limetokana na kazi mbalimbali za ujenzi zinazoendelea ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara za mradi wa mabasi yaendayo kwa haraka jijini Dar es Salaam, barabara za Iringa – Mafinga, Mwenge – Tegeta, Puge – Tabora, Nzega – Tabora, Isaka – Ushiroombo, Iringa – Dodoma, Kidahwe – Uvinza na barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi – Lamadi.

(vii) Uuzaji wa Bidhaa wa Jumla, Reja Reja na Matengenezo

Shughuli hii inahusu kununua bidhaa zilizozalishwa hapa nchini na zilizoagizwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuuza. Vile vile hujishughulisha na matengenezo ya magari, pikipiki na vifaa vya nyumbani. Shughuli hii iliongezeka kwa kasi ya asilimia 7.0 katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 6.1 kipindi kama hicho mwaka 2012. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa, zilizotengenezwa hapa nchini na zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

(viii) Hoteli na Migahawa

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za malazi, chakula na vinywaji. Huduma za hoteli na migahawa ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 4.2 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 6.4 katika kipindi husika mwaka 2012. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa wageni wa ndani na nje ya nchi. Idadi ya wageni wa ndani iliongezeka na kufikia 180,877 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 kutoka wageni 169,703 waliopata huduma mwaka 2012. Aidha, idadi ya wageni kutoka nje ya nchi iliongezeka na kufikia 210,196 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 kutoka wageni 205,522 waliopata huduma mwaka 2012.

(ix) Usafirishaji na Mawasiliano

Shughuli za Usafirishaji na Mawasiliano zinahusu utoaji wa huduma ya usafiri kwa abiria, usafirishaji na utunzaji wa mizigo, wakati mawasiliano yanahusu huduma za simu na usafirishaji wa barua na vifurushi. Shughuli hii iliongezeka kwa kasi ya asilimia 11.6 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 10.6 iliyofikiwa kipindi kama hicho mwaka 2012. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa idadi ya abiria waliohudumiwa na kuongezeka kwa matumizi ya simu za mkononi.

(x) Huduma za Fedha na Bima

Shughuli hii ya kiuchumi inahusika na utoaji wa huduma za fedha zinazotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, benki za biashara, huduma za bima na maduka ya kubadilisha fedha. Shughuli hii iliongezeka kwa kasi ya asilimia 11.6 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 11.3 iliyofikiwa kipindi kama hicho mwaka 2012. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa amana na mikopo iliyotolewa na benki za biashara na huduma za bima.

(xi) Utawala

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kiutawala, kudumisha amani na ulinzi wa nchi zinazotolewa na Serikali. Shughuli hii ilikua kwa kasi ya asilimia 5.1 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 5.5 iliyofikiwa kipindi husika mwaka 2012. Ukuaji huu ulitokana na kuboreshwa kwa huduma ya ulinzi na usalama iliyotolewa na Serikali kwa umma na kuongezeka kwa mishahara ya watumishi wa sekta ya umma.

(xii) Elimu

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma ya elimu kwa shule za umma na binafsi katika ngazi zote za utoaji elimu. Shughuli hii ilikua kwa kasi ya asilimia 5.4 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 6.7 iliyofikiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi walioandikishwa mwaka 2013 ikilinganishwa na mwaka 2012.

(xiii) Upangishaji Majengo na Shughuli za Biashara

Shughuli hii inahusika na upangishaji majengo kwa ajili ya makazi, biashara na utunzaji bidhaa wakati shughuli za biashara zinahusika na utoaji wa huduma za kitaalamu kama vile za kisheria na uhasibu. Shughuli hii iliongezeka kwa kasi ya asilimia 5.3 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 5.0 iliyofikiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma ya makazi na shughuli za biashara kwa ujumla.

(xiv) Afya na Huduma nyingine za Kijamii na Binafsi

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za afya kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma na za binafsi wakati huduma nyingine za kijamii na binafsi zinahusika na utoaji wa huduma kama vile za kiimani, shughuli za urembo na huduma za maktaba. Shughuli hii ilikua kwa kasi ya asilimia 4.8 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 5.4 iliyofikiwa kipindi husika mwaka 2012. Ukuaji huu ulitokana na kuboreshwa kwa huduma za afya na utoaji wa huduma nyingine za kijamii na binafsi katika kipindi husika.

Imetolewa na:

**Mkurugenzi Mkuu
Ofisi ya Taifa ya Takwimu
24 Januari, 2014**